**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**(DIVISHENI YA ARDHI)**

**KANDA YA TANGA**

**RUFAA YA ARDHI NA. 29 YA MWAKA 2019**

**(Inatokana na Rufaa ya Ardhi Na. 32 ya Mwaka 2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Korogwe huko Korogwe na Mgogoro wa Ardhi Namba 5 wa Mwaka 2017 wa Baraza la Kata ya Mswaha wilayani Korogwe)**

**KATI YA**

**IBRAHIM DAUDI MPESHO .....MRUFANI**

**NA**

**RAMADHANI JUMA NKOBA .....MRUFANIWA**

**HUKUMU**

**A.R. MRUMA, J**

Mrufani Ibrahim Daudi Mpesho alifungua shauri la madai ya Ardhi katika Baraza la Kata ya Mswaha Wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga akimdai Mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba shamba lenye ukubwa wa ekari 2 na nusu ambalo alisema ni shamba lao la urithi (wa familia) lililopo Kijiji cha Maurui.

Kwa mujibu wa maelezo ya Ibrahim Daud Mpesho mbele ya Baraza la Kata, eneo hilo ni eneo la asili la wazee wao ambao waliishi hapo. Aliliambia

Baraza la Kata kuwa katika eneo hilo kulikuwa na Makaburi matano ambapo manne yamefukuliwa limebaki moja. Pia kulikuwa na mti mkubwa wa tambiko ambao ulichomwa moto na mrufaniwa na kwa sasa kuna miti minne ya miembe.

Aliita shahidi mmoja aitwaye Ibrahim Said Gagu ambaye alilieleza Baraza la Kata kuwa baba yake aliuziwa shamba eneo hilo la familia ya kina Daudi Mpesho hivyo shamba lao linapakana na akina Daudi Mpesho.

Wakati alipohojiwa na wajumbe wa Baraza kuwa alichukua hatua gani baada ya makaburi manne (4) na eneo la mti wa tambiko yalipoharibiwa alijibu kuwa hawakuchukua hatua yeyote. Alipokuwa akijibu swali ni muda gani umepita tangu mrufaniwa (Ramadhani Juma Nkoba) aanze kutumia eneo hilo alisema kuwa ni muda wa miaka 10.

Kwa upande wake mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba aliliambia Baraza la Kata kuwa yeye alilinunua shamba lililoko kwenye mgogoro kutoka kwa Sisilia Luka aliyemuuzia shamba la baba yake mzee Luka lenye ukubwa wa ekari $1^{1/4}$ (ekari moja na robo). Mauziano hayo yalishuhudiwa na Mwenyekiti wa Kijiji Nuhu Mshana, Menyekiti wa Chama, Iddi Mponzi na Christopher Kucas. Aliliambia Baraza kuwa mwezi Agosti mwaka 2016

aliitwa kwenye mgogoro wa shamba hilo hilo na Baraza la Ardhi la Kijiji. Mgogoro huo ulisuluhishwa bila mafanikio ndipo alipoitwa Baraza la Kata kwa ajili shauri hili.

Katika hukumu yake Baraza la Kata liliamua kuwa kwa kuwa eneo lenye mgogoro lilikuwa na sehemu mbili (ambazo Baraza liliziona lilipotembelea eneo la mgogoro). Sehemu ya kwanza ni eneo ambalo lilikuwa linatumiwa na mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba na eneo ambalo lilikuwa halijaendelezwa ambalo Ramadhani Juma Nkoba alikuwa halitumii. Baraza liliamua kuwa mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba abaki na eneo ambalo alikuwa ameliendeleza na eneo ambalo alikuwa hajaliendeleza libaki kwenye umiliki wa Serikali ya Kijiji.

Mrufani hakuridhika. Alikata rufaa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kupinga uamuzi huo akiwa na sabau nne (4) kama zifuatazo:

1. Baraza lilikosea liliposhindwa kuamuru muuzaji wa eneo husika kuunganishwa kwenye kesi kama mdaawa muhimu.
2. Baraza lilikosea liliposhindwa kuona kuwa kulikuwa na ushahidi kuwa mrufani Ibrahimu Daudi Mesho alikuwa akimiliki eneo hilo tangu miaka ya 1960.

3. Baraza lilikosea kwa kushindwa kuona ushahidi mzito wa mrufani badala yake likashawishika na ushahidi dhaifu unaojikanganya wa mrufaniwa.
4. Kwamba Baraza lilikosea na hukumu yake inaonyesha kuwa mwenyekiti na Katibu wa Baraza walikuwa ni wajumbe.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lilikataa rufaa ya mrufani kwa hoja kuwa kwa kuwa ni mrufani aliyefungua shauri katika Baraza la Kata, yeye ndiye alikuwa na wajibu wa kumuunganisha muuzaji wa eneo hilo. Baraza la Wilaya pia lilisema kuwa kwa kuwa alikuwa amelimiliki kwa muda bila bughudha hivyo alikuwa na kinga kwa mujibu wa Sheria ya ukomo ya Mwaka 1971 aya ya 22.

Mrufani hakuridhika na uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na ameleta rufaa katika Mahakama hii akiwa na sababu nne (4) kama ifuatavyo:

1. Kwamba Baraza la Wilaya lilikosea liliposema kuwa kuunganishwa kwa mnunuzi hakukuwa muhimu.

2. Kwamba Baraza la Wilaya lilikosea lilipompa haki mrufaniwa bila kujali kuwa mrufani alikuwa amekaa kwenye eneo hilo tangu miaka ya 1960 akiishi na kuendeleza eneo hilo bila bughudha yeyote.
3. Kwamba Baraza la rufaa la wilaya lilikosea kwa kushindwa kufanya tathmini ya ushahidi ulio wazi wa mrufani uliokuwa unaonyesha kuwa shamba hilo liliuzwa kwa mzee Mwigazi na sio mrufaniwa na eneo lililobaki ni mali ya mamlaka ya Serikali ya Kijiji.
4. Kwamba Baraza la Rufaa la Wilaya lilikosea kukubaliana na uamuzi wa Baraza la Kata ambalo lilikuwa batili.

Rufa hii ilizungumzwa kwa njia ya hoja za maandishi.

Nimezisoma hoja za maandishi za pande zote mbili. Vilevile nimesoma kumbukumbu katika mabaraza yote mawili kuona ushahidi uliotolewa mbele ya Baraza la kata. Kutokana na mazingira ya mgogoro huu, hoja ya kuunganishwa mnunuzi wa shamba husika haina mashiko. Hoja hiyo haina mashiko kwa sababu mrufani Ibrahim Mpesho katika madai yake msingi aliyoyapeleka baraza la Kata alisema kuwa anamlalamikia mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba kwa kuvamia shamba lao la urithi. Kifungu cha 110 (1) cha Sheria ya ushahidi sura ya 6 kinaeleza wazi kuwa mtu anayedai kuwa na haki inayotokana na ukweli fulani ana wajibu wa

kuithibitishia Mahakama juu ya uwepo wa ukweli huo. Katika shauri hili kwa kuwa mrufani alidai kuwa shamba hilo lilikuwa la urithi, basi alikuwa na wajibu wa kuthibitisha kuwa alirithi shamba hilo. Hakuna ushahidi wowote uliopelekwa mbele ya Baraza kuthibitisha kuwa shamba hilo mrufani alirithi kutoka kwa nani. Alichosema mrufani ni kwamba kulikuwa na makaburi matano bila kueleza yalikuwa makaburi ya nani na hao waliozikwa hapo anahusiana nao vipi.

Kifungu cha 112 cha Sheria ya ushahidi sura ya 6, kinaweka wajibu wa kuthibitisha jambo kwa yule anayetuhumu. Kwa kuwa mrufani ndiye aliyesema alirithi shamba hilo, basi alikuwa na wajibu wa kuthibitisha alirithi kutoka kwa nani na lini. Kusema tu kuwa kulikuwa na makaburi matano (5) na mti mkubwa wa kutambikia hakuthibitishi urithi wa shamba.

Pili, kumbumbumbu zinaonyesha kuwa mrufani Ibrahimu Daudi Mpesho ndiye aliyefungua madai katika Baraza la Kata. Kwa maana hiyo yeye ndiye aliyeamua kwamba amshtaki nani hivyo haiwezi kuwa na hoja kuwa mdaiwa muhimu (necessary party) hakuunganishwa kwenye kesi hii. Alitegemea nani amshtaki muuzaji? Anaweza kusema kuwa hakujua (wakati wa kufungua kesi), kuwa mrufaniwa angekuja na hoja ya kuwa amenunua shamba hilo, lakini kumbukumbu zinaonyesha kuwa mrufaniwa

katika maelezo yake aliyoyatoa mbele ya Baraza la Kata tarehe 25/07/2017 alieleza dhahiri kuwa alinunua ekari moja na robo toka kwa mzee Luka kupitia kwa binti yake aitwaye Sisilia Luka. Baada ya kujua kuwa mrufaniwa anadai kununua na kumtaja muuzaji, mrufani angeweza kuliomba Baraza la Kata ili aweze kumuunganisha muuzaji kama mdaiwa kwenye shauri hili. Hakufanya hivyo, kwa hiyo hawezi kulaumu mtu yeyote kwa kutounganishwa kwa muuzaji. Yeye ndiye alipaswa kumuunganisha mtu yeyote ambaye anadhani kuwa ni muhimu na ana madai dhidi yake.

Kuhusu sababu ya tatu inayolaumu mabaraza ya chini kwa kushindwa kufanya tathimini ya ushahidi kuhusu mrufani kuwa katika eneo hilo kuanzia miaka ya 1960, nimepitia tena ushahidi wa mrufani (Ibrahim Daudi Mpesho) na ule wa shahidi wake Ibrahim Said Guga. Hakuna sehemu yoyote katika ushahidi wao walipotoa ushahidi kuthibitisha au hata kueleza tu kuwa mrufani alikuwa kwenye eneo lile kuanzia mwaka gani. Wakati akitoa ushahidi wake mwaka 2017, Ibrahim Daudi Mpesho (Mrufani) alikuwa na umri wa miaka 46. Hii ina maana alizaliwa Mwaka 1971 (i.e. 2017 – 46 = 1971). Kwa hiyo hoja ya kumiliki eneo lile tangu miaka ya 1960 sio ya kweli na kama alikuwa na maana kuwa familia yake ilimiliki eneo hilo tangu miaka hiyo, basi alipaswa kuita shahidi wa kuthibitisha

jambo hilo. Shahidi wake Ibrahim Saidi Guga yeye alichoeleza baraza ni kuwa yeye baba yake aliuziwa shamba na familia ya Daudi Mpesho na akaeleza mipaka yake. Hakueleza chochote kuhusu mgogoro kati ya mrufani Ibrahimu Daudi Mpesho na mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba. Pia hakueleza ni lini baba yake aliuziwa shamba na familia ya Daudi Mpesho jambo ambalo pengine lingesaidia hoja ya lini mrufani na familia yake walianza kuishi eneo lile.

Kuhusu ubatili wa Mwenendo wa Shauri kwa kuwa Katibu ameingizwa kwenye akidi ya wajumbe wa Baraza la Kata kinyume na matakwa ya kifungu cha 4 (3) cha Sheria ya Mabaraza ya Kata, 1985. Nimepitia Kumbukumbu za Baraza la Kata na hakuna ushahidi wowote kuwa Katibu alishiriki kutoa uamuzi, kuwepo kwa jina lake kwenye akidi ya Baraza la Kata ni sahihi kwani kwa mujibu wa Sheria yeye ndiye anayeandika na kutunza kumbukumbu zote za Baraza. Kwa kuwa imeonyeshwa dhahiri kwenye akidi kuwa yeye ni Katibu, na kwa kuwa kazi za Katibu zinafahamika kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata, mtu anayedai kuwa amefanya kazi nyingine (mfano kutoa uamuzi) ana wajibu wa kuthibitisha hivyo, vinginevyo ni sahihi jina lake na cheo chake kuonekana

kwenye akidi ili kuthibitisha kuwa yeye ndiye aliyeandika kumbukumbu za baraza kama inavyotakiwa na sheria.

Kwa hoja hizo hapo juu, naona rufaa ya mrufani Ibrahimu Daudi Mpesho haina mashiko. Naikataa, na yeye mrufani Ibrahim Daudi Mpesho atamlipa mrufaniwa Ramadhani Juma Nkoba gharama alizotumia kuendesha rufaa hii.

**A.R. MRUMA**

**JAJI**

**12/03/2021**